**HOTUBA YA KAIMU WAKILI MKUU WA SERIKALI NDUGU. MARK MULWAMBO KATIKA KIKAO CHA PILI CHA BARAZA LA PILI LA WAFANYAKAZI OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024, KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA NSSF, MOROGOROTAREHE 19 APRILI, 2024**

**Mhe. Jumanne Abdallah Sagini (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Alice  Edward Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Mteule;**

**Bi. Zuhura Mohamed Kussaga, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Stanley Jennily Mahenge, Naibu Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mtani Melckzedeck Songorwa, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Sarah Rwezaula, Katibu wa TUGHE Ngazi ya Mkoa Dar es Salaam;**

**Bw. Nsubisi Mwasandenge, Mwakilishi wa TUGHE Taifa;**

**Viongozi wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana, Habari za Asubuhi.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, SOLIDARIIIIIITY;**

**MSHIKAMANOOO.**

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha wote kukutana siku hii ya leo tukiwa na afya njema. Pia ninayofuraha kubwa kupata fursa hii ya kuhudhuria Baraza hili la Wafanyakazi likiwa ni Baraza langu la pili kuhudhuria nikiwa kama Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Pili, napenda kutumia fursa hii kuwatambulisha kwako wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi hili ambapo kuna jumla ya wajumbe 42 ambapo wajumbe wanaoingia kwa nyadhifa zao ambao ni Wakuu wa Idara na Vitengo wapo 12, wajumbe wa Halmashauri ya TUGHE Tawi wapo 10, wajumbe wa kuchaguliwa na wafanyakazi wenyewe kwa kila Idara, Vitengo na Ofisi za Mikoani wapo 18, mjumbe mmoja (1) kutoka Baraza

Kuu la Wafanyakazi Serikalini na mjumbe mmoja (1) kutoka TUGHE Mkoa. Vile vile tuna Katibu wa Baraza, Katibu Msaidizi wa Baraza, Sekretariet na Waalikwa mbalimbali.

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Nipende kutumia fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kukubali jukumu hili kubwa la kuweza kumwakilisha Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Binafsi nakupongeza sana Mhe. kwa kuendelea kuamininiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kumsaidia na hatimaye kukuteua kua Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria. Kwetu sisi kama Ofisi, tunatambua kwamba wewe pamoja na Mhe. Waziri mtaendelea kuilea na kuisaidia Ofisi kuweza kufikia malengo yake kupitia miongozo na maelekezo mbalimbali mtakayoyatoa

Nipende pia kumshukuru kiongozi wangu, Dkt Boniphace Luhende (WMS) kwa ushirikiano na miongozo yake aliyonipatia kwa kipindi chote nilichotumika kama Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi OWMS. Nitaendelea kumpatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa mustakabali wa Ofisi yetu.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza **Bi. Alice Edward Mtulo** kwa kuaminiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

kuteuliwa kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali (NWMS) na kuchukua nafasi iliyokuwa imeachwa na **Bi. Sarah Duncan Mwaipopo**. Uteuzi huu uliofanywa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan tarehe 4 Aprili, 2024 ni ishara ya imani kubwa ambayo Mhe. Rais ameionesha kwa watumishi wa OWMS ni dhahiri kuwa ofisi imekuwa na ina uwezo wa kutengeneza viongozi wenye uwezo wa kushika nafasi kubwa kama hii. Nakupongeza sana Bi.**Alice Mtulo**.

Ninakuahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja na tutakuwa bega kwa bega ili kuleta tija kwa ajili ya maslahi mapana ya Ofisi na Nchi yetu kwa ujumla. Hongera Sana.

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

OWMS kwa kutambua na kukidhi takwa la kisheria la kuwepo kwa Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi, imekuwa ikifanya vikao vyake vya Baraza mara mbili kila Mwaka. Baraza hili linawashirikisha viongozi wa TUGHE Tawi, wajumbe wa menejimenti pamoja na wawakilishi wa wafanyakazi kutoka katika Idara na Vitengo kwa kuzingatia muundo wa mkataba wa Baraza. Pamoja na wajumbe hao naomba utambue uwepo wa Sekretariati yetu ambayo inatusaidia kufanikisha mkutano huu.

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Mkutano huu wa Baraza ulitanguliwa na Mafunzo kwa wajumbe wa Baraza yaliyofanyika siku ya jana tarehe 18/4/2024 na kufunguliwa na Mwenyekiti wa Baraza, Mhe. Dkt.Boniphace Luhende. Katika mafunzo hayo, wajumbe walifundishwa mada kuhusu Sheria zinazosimamia Utumishi wa Umma, Haki na Wajibu wa Mtumishi wa Umma mada iliyowasilishwa na **Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** na mada kuhusu Uendeshwaji wa Baraza la Wafanyakazi Mahala pa Kazi mada hii iliwasilishwa na **Ofisi ya Kamishna wa Kazi**

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Hiki ni Kikao cha Pili cha Baraza la Pili la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024**. Kikao hiki ni utekelezaji wa takwa la kisheria la kuwashirikisha Wafanyakazi katika Uongozi wa pamoja mahala pa Kazi, rejea Kanuni Na. 108 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003, Kifungu Na. 73 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004, Kifungu Na. 30 (3) cha Sheria ya Majadiliano ya Pamoja na Kanuni Na. 24 ya Kanuni za Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2005.

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Matunda ya kuwa na Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi yanaendelea kuonekana ndani ya OWMS. Matunda hayo ni pamoja na kuwashirikisha wafanyakazi katika kutoa maoni na kuwasilisha changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi kupitia vikao vya idara, vikao vya wafanyakazi wote pamoja na vikao vingine vya kisheria kama Baraza la wafanyakazi ili kuboresha utendaji na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya OWMS. Pamoja na mambo mengine, madhumuni ya mkutano huu ni kuwawezesha wafanyakazi kupitia Mpango na Bajeti kwa **Mwaka wa Fedha 2024/2025** ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya Bajeti ya OWMS.

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Kwa muktadha huu, Baraza hili litajadili makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha **2024/2025**, ambapo makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka huo ni **Shilingi 20,750,720,000.** Ofisi inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi 4,304,051,000** kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi waliopo na wale watakaoajiriwa, na kiasi cha **Shilingi 16,446,669,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mhe. Mgeni Rasmi** ;

Baada ya kusema hayo, naomba nimkaribishe Mwenyekiti, Wakili Mkuu wa Serikali ili aweze kuzungumza na kukukaribisha ili uweze kuzungumza na wajumbe wa Baraza na hatimaye akukaribishe Mhe. Mgeni rasmi ili uje kutufungulia kikao chetu.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**